

Learning by Ear

People Who Make a Difference

Kenya: Kakamega Educational Environment Programme, KEEP

Author: Josephat Charo, DW Kisuaheli

Editor: Daniel Pelz/ Stefanie Duckstein

Translator: Tony Dunham

Sound clips in DALET: Learning by Ear: [PEO BIOTA_xxx](#)

Characters:

1 Narrator, male or female

5 Voiceovers

- **Emily Mujinji**, female, 23
- **Mildred Atamba**, female, 19
- **Bulinya Atwoli**, male, 20
- **Wycliff Atukha**, male, 25
- **Jared Otieno**, male, 18
- **Mildred Mateche**, female, 19

Introduction (Announcer):

Karibu kwenye kipindi kingine cha Noa Bongo jenga maisha Yako kwa jina watu wanaoleta mabadiliko'. Leo tunawaletea kisa cha msichana mwenye kupenda sana maswala yanayohusiana na mazingira.

Anatumia muda wake mwingi maishani kuilinda miti pamoja na wanyama. Amewashawishi vijana wenzake wakike nao wajiunge kwenye kikundi chake cha vijana kinachotoa elimu ya mazingira cha Kakamega

Environmental Education Programme, KEEP kwa kifupi. Hebu tumtembelee katika msitu wa Kakamega huko magharibi mwa Kenya.

1. SFX Forest birds

2. Soundclip Emily Mujini (English)

“Jina langu ni Emily Mujinji. Niliamua kujiunga na KEEP kwa sababu kabla ya kujiunga nilikuwa namsaidia mtafiti mmoja aliyekuwa akifanya utafiti juu ya kima halafu Jumamosi moja niliwakuta watoto hapa wakijifunza, nilivutiwa sana na kutaka kuwafundisha juu ya mazingira na mimi kujifunza mengi juu ya uhifadhi wa msitu wa Kakamega.”

3. Narrator

Emily ana miaka 23, anatokea Kakamega, mji ulio magharibi mwa Kenya. Yeye ni mwanachama wa kujitolea wa mpango unaotoa elimu ya mazingira mjini Kakamega, unaojulikana kwa kifupi kama KEEP. Emily anasimamia sehemu za malazi katika msitu huo na analipwa posho ya kama Euro 20 kwa mwezi. KEEP iliundwa mwaka 1995 na kundi la waongozaji wa msitu chini ya usimamizi wake Wilberforce Okeka. Ni kikundi cha vijana kinachojihusisha na kazi za kulinda mimea na wanyama katika msitu wa Kakamega kwa lengo la kutoa maelezo kuhusu msitu wa Kakamega kwa watalii, watafiti, na watoto wa shule. Kuna miradi mingi inayotarajiwa kufanyika. Kuna sehemu ya kufuga vipepeo, sehemu ya kufuga nyoka, sehemu ya kupanda miche ya miti pia kuna mradi wa utafiti wa nyani. Emily huanza siku yake asubuhi mapema katika nyumba ya vipepeo.

4. SFX Butterfly House

5. Soundclip Emily Mujinji (English)

“Hii ni nyumba ya Vipepeo. Tunakwenda msituni kuwanasa vipepeo halafu tunawaleta hapa. Tumepanda mazao haya ya chakula ili vipepeo hawa watage mayai chini ya majani hapa.”

6. Narrator

Nyumba ya vipepeo ina pembe nne. Iko wazi lakini imezibwa na neti nyeusi ili kuwazuia vipepeo wasitoroke. Ardhi imejazwa kwa maua ya rangi ya samawati na manjano ambayo yanafanya mahala hapo kuonekana kama vile msitu mdogo. Katikati kuna sehemu zenye maji ambayo vipepeo wanaweza kunywa. Emily na wanachama wengine wa kikundi cha KEEP hukusanya mayai yaliyotagwa kwenye majani na kuyapeleka mahala palipotengwa kwa ajili ya kuangulia mayai.

Mara tu vipepeo wanapoanza kuruka wanachukuliwa na kurudishwa tena msituni. Kwa kufanya hivyo kikundi cha KEEP kinatimiza hatua ya kulinda aina ya vipepeo ambao wamo hatarini kuangamia. Lakini kuna hasara yake pia: Emily na rafiki zake wanalazika kuwagusa vipepeo kila mara. Wanawake wengi huko magharibi mwa Kenya hawataki kabisa kuwagusa vipepeo, wanasema kuwa ule unga unga unaotoka kwa vipepeo hao unaharibu sana kucha zao – Lakini Emily ilimdibi azowee hali hiyo ya kuwagusa vipepeo.

7. Soundclip Emily Mujinji (English)

“Hapana kwanza nilikuwa nawaogopa lakini baada ya kupata mafunzo, uoga wote ulinitoka. Sasa ninawashika bila wasiwasi na kuwafundisha vijana juu ya vipepeo.”

8. SFX Forest ambience

9. Narrator

Kijana mmoja aliyebahatika kukutana na Emily ni Bulinya Atwoli. Ana miaka 20. Amezaliwa na kukulia mjini Kakamega.

10. Soundclip Bulinya Atwoli (English)

“Emily anafanya kazi kwa bidii, ni mbunifu na ana mawazo tele mapya kuhusu kazi hii ya uhifadhi. Amekuwa mstari wa mbele katika kuwasaidia wavulana na wasichana wadogo ili waelewe umuhimu wa kuhifadhi aina ya vipepeo wanaokabiliwa na hatari ya kuangamia. Ninampenda kwa sababu anawahimiza watu washiriki katika kuyalinda mazingira yetu.”

11. Narrator

Mildred Mateche, rafiki yake Emily ana miaka 19. Anatokea Mumias mji jirani na Kakamega, lakini sasa anaishi mjini Kakamega. Anasema kuwa Emily ni mfano bora kwa wasichana wengi.

12. Soundclip Mildred (English)

“Kusema kweli Emily ni mfano bora wa mafanikio. Yeye ni kioo cha jamii na pia ni mfano wa kuigwa kwa wasichana wengi katika maswala ya uhifadhi wa mazingira. Amewashawishi wasichana wengi ili waweze kujitokeza kwa kujiamini na kujitolea katika shughuli za kuhifadhi mimea na wanyama walio katika maeneo yetu. Nimewahi kumuona akivunjika moyo, hasa pale watu wanapokataa kufanya anachowaambia. Nina maana kuwa yeye hukasirika mara nyingine kama binadamu mwingine yoyote....Si unajua tena.”

13. SFX: Forest

14. Narrator

Msitu wa Kakamega ni wa kipekee nchini Kenya wenye kufanana na aina ya msitu wa Guinea na Kongo; msitu mnene ambao katika millennia iliyopita, ulitanda katika eneo lote la Afrika ya Kati. Kazi ya Emily inahitajika sana msituni. Bila ya kikundi cha KEEP, msitu huo usingekuwepo. Miti ya kijani yenye matawi mapana ya kijani yanayotoa kivuli kwa wanyama wanaokaa chini yake. Wako tumbili, kima, vichakuro na aina tofauti za ndege. Lakini msitu huo unakabiliwa na hatari. Mahitaji ya chakula yanaongezeka kwa idadi kubwa ya watu Magharibi mwa Kenya. Kwa hivyo kila kukicha wakulima wanazidi kuingia msituni na wawindaji haramu nao wanaendelea kuwauwa wanyama kwa ajili ya kuuza nyama yao.

Jambo la kutia moyo ni kwamba, Emily na wanachama wengine wa mradi wa elimu kuhusu mazingira wa Kakamega hawako peke yao kwenye harakati za kuhifadhi msitu. Wanaungwa mkono na shirika la BIOTA, (**Inatamkwa Bayota**) shirika linalo simamia utajiri asilia na wanyama pori barani Afrika kwa kutoa msaada wa kisayansi kwa matumizi na uhifadhi wa Bio anuai barani Afrika; Emily anafurahi kuwepo shirika la BIOTA.

15. Soundclip Emily Mujinji (English)

“BIOTA, ninafhamu kuwa wao ni washirika wetu wakuu na wamekuwa wakifanya kazi katika maeneo ya msitu wa Kakamega, wanafanya utafiti msituni, najua kuwa wamewaajiri baadhi ya wanachama wetu.”

16. SFX Sound of monkeys/ forest ambience

17. Narrator

Mfano mmoja wa matokeo ya ushirika wetu ni huu mradi wa kima. Wanachama wa KEEP wanaingia msituni na kuwatia alama kima na tumbili wote watakaowapata kwa kutumia tabia au sifa bainifu. Hatua hiyo itarahisisha kujua idadi yao itakapoanza kupungua au pia kufuatilia utaratibu wa malisho ya wanyama hao. Vilevile wanaondoa mitego inayowekwa na wawindaji haramu kwa ajili ya kuwatega kima na tumbili. Mildred Atamba mwenye umri wa miaka 19 anasema hiyo si kazi rahisi.

18. Soundclip Mildred Atamba (English)

“Baadhi ya wawindaji haramu wakituona huko msituni wanafirikiria labda tutawakataza kuwinda wanyama na kuchukua nyama, ndio maana wanatupinga na tunapata shida kutoka kwao.”

Mildred anasema kuwa mara nyingine wao hufukuzwa na wawindaji hao haramu, mara nyingine wanakemewa au hata kutishwa kwa sababu ya kuwaondolea mitego yao na pia kuwalinda kima na tumbili wasinaswe na mitego hiyo.

19. SFX Snake laboratory

20. Narrator

Mradi mwingine muhimu ni mahala pa kufugia nyoka. Upande mmoja mahala hapo kuna maabara. Ni chumba kidogo cha mbao ambacho kimepangwa rafu za mbao zilizojaa chupa zenye kemikali. Pembeni kuna chombo kikubwa kilicho wazi na ndani yake mna nyoka mkubwa mwenye madoadoa ya rangi ya kijivu na nyeusi amerowanishwa kwa kemikali. Nyoka waliokufa huhifadhiwa kwa ajili ya mafunzo kwa jamii. Wycliffe Atukha, mwenye umri wa miaka 25, ni msimamizi wa sehemu

hii ya kufugia nyoka katika mradi wa KEEP. Anasema kuna aina 40 za nyoka kaatika msitu wa Kakamega. Anafanya utafiti wa nyoka na anajaribu kuwashawishi wenyeji wawakubali nyoka na kuishi pamoja nao. Kwa muda mrefu wenyeji wanaopakana na msitu wa Kakamega wamekuwa wakiwaua nyoka kwa sababu wanaamini kuwa nyoka ni wabaya. Elimu kabambe inayotolewa na mradi wa KEEP imeanza kubadili mtazamo huo.

21. Soundclip Wycliffe Atukha (English)

“Nimegundua kuwa sasa watu wameanza kubadili mtazamo wao. Wameanza kukubali kuwa nyoka sio wanyama wabaya na sasa hawawauwi tena nyoka. Yote haya ni kwa sababu watu wameanza kufahamu zaidi juu ya nyoka. Nina hakika watu wengi wataajiriwa hapa mradi wa kufuga nyoka na watakuwa na uelewa mkubwa kuhusu nyoka.”

22. SFX Trees/ Walking on grass and dry branches, sticks

23. Narrator

Mradi mwingine wa KEEP ni mradi wa bustani ya miche ya miti. Wanachama hukusanya mbegu kutoka msituni wakati wa majira ya mvua na kuipanda kwenye bustani. Lengo kuu ni kuhifadhi aina mbalimbali ya miti katika msitu wa Kakamega kwa ajili ya kupata kipato. Jared Otieno, ana miaka 18, na ndie msimamizi wa mradi wa kupanda miti. Anasema changamoto zipo.

24. Soundclip Jared Otieno (English)

“Kuna wadudu wengine ambao kwa kawaida wanashambulia miche katika bustani, na zaidi ya miche hiyo ni chakula cha baadhi ya vipepeo.”

Kwa hivyo tukinyunyizia dawa za wadudu tunahofia vipepeo watakula miche na kufa.”

25. Narrator

Emily anawaandaa wengine kufuata nyayo zake katika kuleta mabadiliko. Rafiki yake Mildred Mateche anaamini kuwa ni kwa sababu ya watu kama Emily ndio maana msitu wa Kakamega uko salama.

26. Soundclip Mildred Mateche (English)

“Kuwa mtu kama Emily ambaye amejitolea kwa nguvu na uwezo wake wote kutumia muda wake kufanya kazi kama hii ni changamoto kubwa kwangu. Ananishagaza sana vile anavyoweza kutimiza mambo mengi. Namuonea wivu! Kwa marafiki zake wanaofanya kazi naye kwenye mradi wa KEEP, nasema Hongereni! Mnafanya kazi nzuri. Endeleeni vivyo hivyo! Ninafurahishwa zana na kazi yenu! ”

OUTRO (Announcer):

Ni hayo tu kwa leo kutoka kwenye makala ya Noa Bongo Jenga maisha Yako. Hadithi ya leo imeandikwa na Josephat Charo. Kumbuka kwamba mazingira bora yanahitaji ushirikiano wetu sote. Unaweza kusikiliza tena kipindi hiki kwenye mtandao. Anuani yetu ni www.dw-world.de/lbe hadi wakati mwingine. Kwaheri!

END